TANGAZO LA SERIKALI NA. 701 la tarehe 02 /12/2022

SHERIA YA MIPANGOMIJI,

(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA LOYA YA MWAKA, 2022

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Loya ya Mwaka, 2022.

Kutangazwa kwa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango wa jumla na kina wa eneo

3. Mpango wa jumla na wa kina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Uyui.

**JEDWALI**

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la Upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka L1 iliyopo barabara ya Marongwe Kusini - Magharibi mwa makazi ya mtaa wa Mlimani katika majira-nukta 591809E, 9440551N; baada ya hapo mpaka utaendelea Magharibi - Kaskazini katika uelekeo wa W155$^0$10'20" kwa umbali wa kilomita 2 hadi alama ya mpaka L2 iliyopo pembezoni mwa mto Ng'wale kwenye majira-nukta 589843E, 9441491N; baada ya hapo mpaka utafuata mto Ng'wale Kaskazini - Mashariki hadi katika alama ya mpaka L3 yenye majira-nukta 594145E, 9444282N Kaskazini mwa Makazi ya Loya; baada ya hapo mpaka utafuata Mashariki - Kusini katika uelekeo wa E125$^0$8'20" kwa umbali wa kilomita 1.5 hadi alama ya mpaka L4 iliyopo barabara ya mbugani yenye majira-nukta 595362E, 9442785N; baada ya hapo mpaka utaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa S90$^0$6'0"W kwa umbali wa kilomita 2.2 hadi alama ya mpaka L5 iliyopo Kusini mwa makazi ya Loya katika barabara ya Migogwa yenye majira-nukta 593113E, 9440829N; baada ya hapo mpaka utaelekea Magharibi-Kaskazini katika uelekeo wa W160$^0$10'40"N kwa umbali wa kilomita 2 hadi ulipoanzia"

Dodoma,
8 Novemba, 2022

ANGELINE S. MABULA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*